**IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH**
**(ISSN: 2805-413X)** **Dkt. Jackline Murimi***

https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*
*Mitindo Iliyotumiwa Kufanikisha Uwasilishaji wa Mashairi Teule katika Diwani ''Nachora kwa Maneno''na '' Mashairi ya Wanyama"*

# Mitindo Iliyotumiwa Kufanikisha Uwasilishaji wa Mashairi Teule katika Diwani ''Nachora kwa Maneno''na '' Mashairi ya Wanyama"

**Dkt. Jackline Murimi**

Mhadhiri katika Idara ya Lugha na Isimu,Chuo Kikuu cha Tom mboya

na

**Katunda Charo James**

Mwanafunzi Idara ya Elimu Jamii, Chuo Kikuu cha Mount Kenya

## IKISIRI

Malengo ya utafiti huu yalikuwa ni kuchambua maudhui ya mashairi hayo, kutathmini wahusika na kukagua *m*.

**Maneno Muhimu**: ***Mitindo, Mashairi Teule***, ***Nachora kwa Maneno, Mashairi ya Wanyama,***

## Usuli wa utafiti

Maudhui ni mkusanyiko wa ujumbe na mawazo tofauti yanayojitokeza katika shairi fulani. Haya ni mambo yanayojadiliwa katika shairi, na yanaweza kuwa na mawazo mbalimbali. Maudhui husaidia kuunda dhamira ya shairi hilo, ambapo dhamira inamaanisha lengo, madhumuni, au nia ya mwandishi wa shairi.Ndani ya fasihi ya watoto tunapata mashairi ya watoto. Diwani "Nachora kwa maneno ya Swaleh Mdoe na mashairi ya wanyama ya Ali Hassan Kauleni na Elvera Shabiha ni diwani za mashairi ya watoto zinazotumika kufunza lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Fasihi ya watoto ina sifa maalum zinazoiweka wazi. Kulingana na Wamitila (2008), sifa hizi ni pamoja na matumizi ya michoro yenye mvuto na ubora, lugha rahisi inayoweza kueleweka na watoto, na uwepo wa fantasia. Mara nyingi, wahusika wakuu katika fasihi ya watoto ni watoto wenyewe, na simulizi hizi hufungamana na motifu ya safari na msuko. Pia, fasihi ya watoto ina muundo rahisi, si mrefu sana, na huzingatia saikolojia ya watoto. Sifa hizi zinatokana na umri wa hadhira inayolengwa. Wamitila (2008) anabainisha kwamba fasihi ya watoto inavyoathiriwa na mtazamo wa jamii kuhusu watoto, na itikadi hii inaathiri jinsi tunavyoteua kazi za fasihi na matarajio yetu kuhusu kazi hizo, ikiwa ni pamoja na uandishi, dhamira, wahusika, na mwelekeo wake. Fasihi ya watoto inajumuisha nyimbo, mashairi, methali, vitendawili, ngano, hadithi fupi, na riwaya.

Fasihi ya watoto husaidia kukuza matumizi ya lugha. Mtoto anaposoma shairi, hujifunza msamiati mpya anaoweza kutumia katika mawasiliano yake ya kila siku. Shabaha za fasihi ya watoto ni kumwezesha mtoto kuingiliana vyema na wanajamii wengine. Aidha, inamsaidia mtoto kuzijua na kuzitukuza amali, hivyo kumpa msingi bora wa kuwa na sifa kamili za utu.

Ushairi ni sehemu ya fasihi inayotumia mpangilio maalum wa lugha, picha, na mapigo yaliyokusudiwa ili kueleza maudhui. Vigezo vinavyotumika kuchambua na kuainisha ushairi ni umbo lake pamoja na matumizi ya lugha. Kulingana na Senkoro (1982), ushairi hutumia lugha ya mkato inayotoa maudhui kwa muhtasari na mara nyingi huficha maudhui haya ndani ya taswira na ishara. King'ei (2000) anasema kwamba ushairi ni sanaa inayotumia lugha ya muhtasari iliyochanganuliwa kwa njia ya kiufundi ili kufanikisha athari iliyokusudiwa. Ameonyesha kuwa miundo ya mashairi hubadilika kulingana na mpito wa wakati, na ndiyo sababu mashairi kama utenzi, takhmisa, hamziya, na tumbuizo yanayofungamana na maudhui hayaandikwi kwa wingi.

Kila kazi ya fasihi ya watoto ina maudhui. Maudhui ndio ujumbe uliolengwa na mshairi katika kila shairi. Maudhui ya mashairi ya watoto yana maudhui yanayorejelea ulimwengu wa mtoto. Kahigi (1995) na mulokozi

(1995) wanasema dhana ya ushairi inastahili kuzingatia umbo la ndani yani maudhui ili ujumbe umfikie mlengwa na kumwathiri kwa namna iliyokusudiwa.
Wahusika katika fasihi ya watoto ni sehemu muhimu ya kazi hizo. Wengi huwa watoto au wanyama na hurejelea maisha yao. Huwa hodari au wenye mapungufu yenye mafunzo kwa watoto. Kulingana na Bakize (2014), kwa kuwahusisha watoto, mtunzi anawapa nafasi ya kujitazama wenyewe kimatendo na hivyo kujirekebisha pale wanapokosa. Kwa hivyo, ni muhimu kutathmini wahusika wa mashairi.

Kwa mujibu wa Ngugi (2009) watoto husoma ili waweze kupata kukuza kipawa cha lugha, kuimarisha ubunifu wao pamoja na kujiepusha na tabia hasi. Hivyo mtindo wa mwandishi huchangia mashairi ya watoto kuufikisha ujumbe kwa hadhira. Hivyo kunahaja kuchanganua mtindo wa uandishi wa mashairi. Kipengele cha lugha ni zana muhimu katika kufaulisha kazi ya sanaa hususan mashairi ya watoto.

**Suala la Utafiti**

Suala la utafiti huu linahusisha kuchanganua mitindo iliyotumiwa kufanikisha uwasilishaji wa mashairi teule katika diwani za "Nachora kwa Maneno" na "Mashairi ya Wanyama." Lengo ni kuelewa jinsi mitindo mbalimbali inavyoathiri maudhui na ujumbe wa mashairi ya watoto. Utafiti utaangazia matumizi ya lugha rahisi na yenye mvuto, pamoja na mbinu za kihisia kama taswira na picha zinazotumiwa na waandishi. Aidha, muundo wa mashairi, ikijumuisha vina na mahadhi, utachambuliwa ili kuona jinsi unavyochangia katika uwasilishaji wa ujumbe. Wahusika, hasa watoto na wanyama, watachunguzwa ili kuelewa jinsi wanavyoakisi maadili na tabia zinazohusiana na ulimwengu wa watoto. Utafiti pia utaangazia athari za mitindo kwa watoto, ikiwa ni pamoja na kukuza uwezo wa lugha na kuvutia hamasa ya kusoma. Kwa hivyo, suala la utafiti linatoa mwanga juu ya jinsi mitindo ya uandishi inavyoweza kufanikisha uwasilishaji wa mashairi, na jinsi inavyoweza kuathiri watoto katika kujifunza na kukuza maadili. Utafiti huu unatarajiwa kutoa mchango muhimu katika kuelewa umuhimu wa ushairi wa watoto.

**Lengo la Utafiti**

Kuchanganua mitindo iliyotumiwa kufanikisha uwasilishaji wa mashairi teule katika diwani ''Nachora kwa maneno''na '' Mashairi ya Wanyama

**Umuhimu wa Utafiti**

Ukuzaji wa Fasihi ya Watoto: Utafiti ulijikita katika ushairi wa watoto ili kuwahimiza waandishi kutoa machapisho zaidi katika eneo hili. Hili limeshughulikia tatizo la upungufu wa fasihi ya watoto, kama alivyobainishwa na Bakize (2014). Hii itasababisha maendeleo ya fasihi ya watoto katika eneo hili.

Uboreshaji wa Utamaduni wa Kusoma: Pia unalenga kuboresha utamaduni wa kusoma kwa watoto katika usomaji wa vitabu, hasa vitabu vya ziada, kama anavyobainisha Nyaga (1988), kupitia uchambuzi wa mashairi ya watoto na uwezo wao wa kuwavutia watoto kusoma badala ya kutazama runinga na. aina nyinginezo za burudani.

Uboreshaji wa Nyenzo za Kufundishia: Kwa kuchunguza maudhui, wahusika, na mbinu za kimaandishi zinazotumiwa katika ushairi wa watoto, utafiti huu utatoa vidokezo mbalimbali kwa walimu na waandishi. Hii ingetokeza nyenzo za kufundishia zenye kuthawabisha zaidi kwa watoto.

Ukuzaji wa Uwezo wa Kiakili: Utafiti unaonyesha nafasi ambayo ushairi hucheza katika ukuzaji wa uwezo wa kiakili wa watoto. Kwa hili, Ruthiiri (2012) anataja kuwa ushairi huwa na ufanisi katika kukuza uwezo wa

kiakili wa watoto. Unajipanga kuonyesha jinsi ushairi unavyoweza kuwa msaada katika kuimarisha fikra za watoto, ubunifu, na utambuzi.

Kukuza Maadili na Utamaduni: Kupitia uchanganuzi wa maadili hasi na chanya katika mashairi ya watoto, utafiti utahamia kwenye elimu ya maadili ya watoto ili kuwaongoza kuelekea wema. Hii itaboresha uelewa wa kitamaduni kupitia ukuzaji wa mashairi ambayo yanajumuisha mazingira na maisha ya watoto kama vile Gituku alisema mnamo 1990.

Mchango katika Utafiti wa Fasihi na Elimu: Utafiti huu ni mchango muhimu, asemavyo Laurent (2024), katika utambuzi wa utafiti wa sasa wa fasihi na elimu, huku ukifungua mitazamo mipya kuhusiana na umuhimu wa ushairi wa watoto katika ujifunzaji na maendeleo. Unaweza pia kufungua njia ya masomo zaidi juu ya athari za elimu na fasihi ya watoto.

**Uhakiki wa Fasihi**

**Mtindo Katika Mashairi ya Watoto**

Kuchanganua mtindo katika kazi ya fasihi kunahitaji kuzingatia miundo na vipengele vya lugha vinavyovutia (Coombes, 1953). Coombes anaeleza wazo la kishairi, hisia zilizoibuliwa, uteuzi wa maneno, urari wa vina, and mahadhi ya shairi. Lengo la kimtindo ni kuchunguza lugha na kanuni zake ili kubainisha mbinu na vipengele vinavyotumiwa katika kazi fulani ya jamii, (Ismail, (2019)

Mtindo kwa njia nne kuu wanaelezea Nyutu, (2016) Kwanza, wanaeleza kama tabia ya mtu katika matumizi ya lugha, yaani jinsi mtu anavyotumia lugha kuwasilisha ujumbe wake. Pili, nikuonyesha hulka na upekee wake na tabia ya mtu binafsi kuhusu matumizi ya lugha. Hivyo, wanaafikiana na Buffon, ambaye anasema jinsi mtu anavyoitumia lugha kupitisha ujumbe wake.

Wanaeleza kama jinsi jamii au kikundi fulani wanavyotumia lugha katika kipindi fulani; kama ilivyo kwa mtindo wa mashairi wa "kishujaa" wa Kiingereza cha zamani. Hii ina maana kwamba kuelewa hali pana ya matumizi ya lugha kutatusaidia kuwa waangalifu zaidi katika kuelezea hali ya wanaoshiriki lugha hiyo.

Mtindo pia unarejelewa kama tabia ya kueleza mambo, ikiwa ni pamoja na kusema kwa njia inayofaa au isiyofaa, yaani matumizi sahihi katika mazingira fulani. Kwa mfano, mtindo ulio na hadhi au urembo zaidi. Wanadai kwamba mtindo pia katika fasihi ni kama maandiko bora yenye sifa na urembo.

Nyandiwa, H. (2015). anasema kazi ya fasihi inalenga kuwasilisha hisia au tajiriba kwa wasomaji au wasikilizaji wake. Kwamba mshairi hutumia lugha 'kiajabu,' na kwamba athari za ufumi hazitenganishwi na matumizi ya lugha kisanaa, leech anasema. Kimetto, H. K. (2016), anasema mtindo unahusu sifa za kutumia mpangilio wa lugha mkato, picha, na mapigo maalum, na vigezo vya kuchambua na kubainisha shairi na umbo lake pamoja na matumizi ya lugha. Anongeza kwamba ushairi hutumia lugha ya mkato inayosaidia kuendeleza maudhui kimuhtasari, mara nyingi ikiwa katika kibwagizo.

Yunus, M. K. (2013) wanadai kuwa mtindo ni ufundi wa kupanga na kujieleza, na kwamba mtindo hutofautisha mtunzi mmoja na mwingine. Mtindo ni jinsi mtunzi anavyotumia lugha katika kujieleza Mbatia (2001). Kulingana na Wamitila (2010), jinsi mwandishi anavyojieleza katika kazi yake, mtindo ni sifa, fani, au miundo inayobainisha kazi fulani maalum au mtunzi maalum. Hivyo, mtindo unaweza pia kuwa wa wakati fulani au eneo fulani. Hii, nadharia hii inajikita kwenye uchanganuzi wa lugha kwa kiasi

kikubwa, na uchunguzi huu unapania kubainisha ubunifu ulio katika lugha hiyo, ambao kwa kuutekeleza kwa undani, unasaidia katika uelewa wa mashairi.

Kwa mujibu wa childs na fowler (2006) hii ni njia ya kujieleza, ifafanuliwayo kiisimu lakini inayothibitika na kupimika kwa kutumia vigezo visivyo vya kiisimu. Kijelezi hiki ndicho hufanya dhana hii kuwa tata kwa kuwa kuhusu matumizi ya mambo yasiyo ya kwenye muundo wa mawasiliano hupangwa kimfumo, kisha mfumo huo kusababisha na seti maalum ya vipengele vilivyo nje ya matamshi Wamitila, (2008). Huu ubainishi wa mtindo kwa kutumia muktadha hujitokeza ndani nan je ya fasihi. Hivyo basi mitindo yaweza kuangaliwa na mhusika kujieleza katika hali hii, mtindo humpambanua mtunzi mmoja na mwingine, neno moja na jingine, tapo moja na jingine, utanzu na mwingine au kipindi na kingine. Huwa ni upekee kazi fulani usioweza kuigwa.

## Misingi ya Nadharia

### Nadharia ya Kimtindo

Nadharia ya kimtindo ina chimbuko lake katika kundi la Kiisimu la Moscow, hasa Viktor Shyklovsky, mwanzoni mwa karne ya 20. Iliasisiwa itumiwe kuelezea kuwa fasihi ni matumizi ya pekee ya lugha, tofauti na lugha ya kawaida. Baadhi ya waandishi muhimu katika eneo hili ni pamoja na Coombes (1953) na Leech (1979). Coombes anasema kwamba ili kuchanganua mtindo katika kazi ya fasihi, ni muhimu kuzingatia vipengele vinavyovutia kazi hizo. Vipengele hivi ni pamoja na matumizi ya taswira, wazo la kishairi, hisia zinazoibuliwa, uteuzi wa maneno, urari wa vina, na mahadhi ya shairi. Vipengele hivi vya matumizi ya lugha ndivyo humwezesha msomaji kuukadiria umaarufu wa mwandishi na fasihi haiwezi kuchunguzwa bila kuzingatia ya lugha. Hii kulingana na Wamitila (2003) kwamba kazi ya kifasihi ndiyo hupewa umuhimu mkubwa kuliko mtunzi wake kwa kusisitiza umuhimu wa lugha katika kuelezea maana ya fasihi.
Nadharia ya kimtindo inategemea dhana kwamba lugha ina mchango mkubwa katika kufanikisha kazi ya sanaa. Inasisitiza kwamba kazi ya fasihi haiwezi kueleweka bila lugha. Jinsi mtunzi anavyotumia lugha ni muhimu kwa kueleweka kwa kazi hiyo, na hivyo ujumbe wa kazi unaweza kufikia hadhira. Hii inathibitishwa na Tutas (2006) akirejelewa na Timucin (2010). Lugha ndicho chombo muhimu zaidi cha alichonacho mwandishi cha kuwasilishia mawazo yake kwa hadhira (Mwangi, & Munyao, 2016).
Kwa hivyo, ili kuyaelewa maudhui ya ushairi, kuna haja kuchaguza, kuchanganua na kuielewa lugha iliyotumika. Hii ina maana kwamba mtindo wa shairi ndio njia kuu ya kuyafikia maudhui yake. Katika hali hii, nadharia ya kimtindo hufaa kuyachunguzia mashairi. Hii ni nadharia inayosisitiza matumizi ya mbinu za kisayansi zilizopo katika taaluma ya isimu kuchahanuliwa matini za kifasihi. (Stephano, 2022)
Lengo hasa la uchanganuzi wa kimtindo basi huwa kubainisha jinsi muundo wa kiisimu unahusiana na athari ya kifasihi iliyomo kwenye matini.Lugha ni kipengele cha kimsingi cha kuiunda na kuifanya kazi ya fasihi kueleweka. Kupimiwa ubora wake na kuiwezesha kuwepo (Nguti, 2013). Bila lugha hakuna fasihi. Nadharia ya kimtindo hudhamiria kufanikisha uchunguzi wa kina wa matumizi ya lugha katika fasihi. Lugha ina matumizi ya kawaida na ya kisanii. Katika matumizi ya kawaida au umbo la ndani, kuna tamathali za usemi na upotoshi wa lugha kimakusudi. Utafiti huu utafaidi kutoka kwa mawazo ya Leech kuhusu namna ya kushughulikia mtindo ambao umefumwa katika matumizi ya lugha, wahusika na miundo ya sentensi.
Katika nadharia hii, lugha ya kishairi hutambuliwa kutokana na matumizi yake kisanaa, hali ambayo inarejelewa na Wamitila (2003) kama ufasihi, dhana inayofafanuliwa na Mbatia akirejelewa na Gituru, (2019), kuwa ni matumizi ya kipekee ya lugha. Kupitia kwa ufasihi, msomaji hupata maana ya fasihi

iliyoundwa kwa kuzingatia matini zenyewe. Huu upekee hujitokeza kupitia ukiushi wa viwango mbalimbali unaojitokeza kupitia uhuru alio nao msanii.

**Mihimili ya Nadharia ya Kimtindo**

i. Lugha kama chombo tekelezi huwa muhimu katika kuuelewa ujumbe uliokusudiwa. Mhimili huu ulitusaidia kubaini vipengele vya lugha vilivyotumiwa katika kuyawasilisha maudhui ya mashairi teule.
ii. Uwiano kati ya ujumbe na lugha huchangia ufanisi wa kazi ya sanaa kwa sababu hutumika katika uzuaji na ubunifu wa kifasihi. Kwa mfano, jinsi mtunzi anavyounganisha tukio moja na lingine, wazo moja na lingine au mshororo mmoja na mwingine.
iii. Mihimili ilisaidia kuelewa mtiririko wa habari katika ushairi wa watoto ili kufanikisha uwasilishaji wa maudhui.
iv. Kazi ya sanaa huwa na sehemu kama ploti, dhamira, maudhui na wahusika lakini bila lugha vipengele hivi haviwezi kuwasilishwa vilivyo. Sehemu hizi hupewa umbo kupitia lugha. Mhimili huu utatusaidia kuelewa muundo wa mashairi husika kama kijenzi cha mtindo. Muundo huo katika mashairi yaliyoshughulikiwa una vipengele vingi kama vile picha, wahusika na mpangilio wa vitushi.

**Mbinu ya Utafiti**

Utafiti huu unalenga kuchanganua ushairi wa watoto kwa kuzingatia maudhui, wahusika, na mitindo iliyotumika katika diwani mbili teule. Kulingana na Kothari (2008), muundo wa utafiti hutoa mwongozo wa jumla kuhusu jinsi utafiti unavyofanyika kutoka mwanzo hadi mwisho. Katika utafiti huu, muundo wa kiuchanganuzi ulitumika ambapo mashairi kutoka diwani "Nachora kwa Maneno" na "Mashairi ya Wanyama" yalichambuliwa maktabani. Uchanganuzi huu ulilenga kuelewa jinsi waandishi walivyowasilisha maudhui ya watoto kwa kutumia mbinu na mitindo tofauti. Mtafiti alilenga kutoa mwangaza zaidi juu ya jinsi ushairi wa watoto unavyoweza kuchangia katika fasihi ya watoto kwa ujumla, hivyo kufanikisha malengo ya utafiti huu.

Katika uchunguzi wa data, usampuli wa kujitolea ulichukuliwa, ambapo mashairi kumi yaliacha mkato kutoka kwa diwani mbili zilizoteuliwa kwa uchunguzi mpana. Mashairi matano yalichukuliwa kutoka diwani "Nachora kwa Maneno" na mengine matano kutoka diwani "Mashairi ya Wanyama." Mbinu hii ya sampuli ilitengenezwa kwa sababu mashairi yaliyomo kwenye diwani zote mbili yalikuwa na uhusiano mkubwa kimaudhui, kimtindo na kimbinu, kwa hiyo yatakuwa katika utafiti mzuri na wa gharama nafuu. Kelly (2010) na Palinkas et al. (2015) wanaeleza kuwa sampuli kusudio husaidia kwa kurahisisha utafiti wa data zinazohusiana. Ukusanyaji wa data ulifanyika kwa kuchambua mashairi husika, ambapo mtafiti alinukuu sehemu maalum zinazohusisha maudhui, wahusika, na mitindo iliyotumika. Utafiti huu ulifanywa maktabani, na vitabu hivyo vilisomwa na kuchambuliwa kwa makini ili kufikia malengo yaliyowekwa.

Mtafiti alichanganua data kwa kutumia mbinu ya uchanganuzi wa yaliyomo. Uchanganuzi wa yaliyomo, kwa mujibu wa Yang (2008), unahusisha uchambuzi wa kiuratibu wa matini iliyoteuliwa kwa kutumia ujumbe rudilifu na halali ili kuelezea masuala yaliyo kwenye matini. Katika utafiti huu, mtafiti aliangazia maudhui mashairi, wahusika, na mitindo ili kubainisha jinsi ambavyo waandishi wa ushairi wa watoto walivyowasilisha vipengele hivi kwa ufanisi. Matokeo ya utafiti yaliwasilishwa kwa njia ya maelezo ya kina, ambapo mtafiti alieleza jinsi maudhui ya mashairi yalivyohusiana na wahusika, mtindo, na matumizi ya lugha. Mbinu hizi za ushairi zilielezewa kwa mifano kutoka kwa mashairi yaliyochaguliwa ili kutoa taswira kamili ya malengo ya utafiti.

Utafiti huu pia uliheshimu maadili ya kitaaluma kwa kuhakikisha kuwa mtafiti alipata kibali na idhini ya kufanya utafiti katika maktaba za vyuo husika. Aidha, hakukuwa na unakili wa kazi za kitaaluma bila idhini;

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Dkt. Jackline Murimi*

https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||



machapisho yote yaliyotumiwa yalitajwa kwa uwazi ili kuhakikisha uaminifu wa kitaaluma. Mtafiti alizingatia sheria na kanuni za utafiti za kitaifa na za chuo, kuhakikisha kuwa matokeo yaliwasilishwa kwa njia ya wazi na inayozingatia viwango vya kitaaluma.

**Matokeo na Majadiliano**

**Sehemu ya Tatu; Mitindo ya Mashairi Teule**

Kulingana na Ntarangwi (2004) lengo la umtindo ni kuona jinsi lugha ilivyotumiwa na kupangwa. Umtindo hudai kuwa kuna athari zilizo nje ya matini kwenye muundo wa mawasiliano hupangwa kimfumo, kisha mfumo huo kusababisha mipangilio ya muundo wa kiisimu ambao huwa wenye utaratibu, na ubainifu, yaani kuwa na seti maalum ya vipengele vilivyo nje ya matamshi Wamitila (2008). Huu ubainishi wa mitindo kwa kutumia muktadha hujitokeza ndani na nje ya fasihi. Mtindo ni upangaji wa fani na maudhui katika kazi ya fasihi kwa namna inayopambanua mtunzi, msomaji, utungo, enzi au eneo. Coombes (1953) na Leech (1969) wanaafikiana kwamba kuchanganua mtindo sharti vipengele vinavyofanya kazi fulani vivutie, na mtunzi hana budi kuonyesha umaarufu wake katika matumizi ya lugha. Katika sehemu hii mtafiti anachanganua mitindo ya mashairi teule. Kwanza mtafiti amechanganua suala la lugha ya mashairi teule, pili toni ya mashairi teule, vielelezo vya picha michoro na rangi, urudiaji, taswira na muundo.

**Lugha ya Mashairi Teule**

Kulingana na nadharia ya kimtindo ,lugha ni mhimili ambao unawezesha kuyaelewa maudhui.Lugha ina nafasi kubwa katika fasihi kwa kuwa fasihi yenyewe ni sanaa ya lugha.Lugha hapa itatumika kwa maana ya mfumo wa ishara ambazo hutumiwa na mtunzi kuwasilisha ujumbe.(TUKI 1990,Delahunty,Garvey2010)Lugha ndiyo malaghafi inayotumika kuubeba ujumbe.Katika kipengele cha lugha mtafiti alichanganua uteuzi wa msamiati wa mashairi teule,tamathali za usemi katika mashairi teule,urari wa vina na mahadhi ya ushairi wa mashairi teule,ukiushi na usambamba.

**Uteuzi wa Msamiati**

Ntarangwi (2004) anasema maneno yanayotumiwa katika fasihi ni maneno zaidi ya maneno mengine kwani yanatumiwa kisanaa. Uteuzi wa msamiati ndio nyenzo ya kimsingi aliyonayo mtunzi. Mtindo mzuri niule ambao maneno halisi yameteuliwa na kuwekwa pamoja kuwa muundo mwema zaidi. Katika shairi" njiwa" kwenye diwani mashairi ya Wanyama watunzi wanarejelea maneno ya kawaida kwa mtoto kama vile, njiwa ambaye kulingana na kamusi ya karne ya 21 ni ndege wa jamii ya tetere au pugu lakini mkubwa anayekula nafaka mwenye rangi ya kijivu na nyeupe iliyopauka. Maneno mengine ni kama vile mpole, wema, duniani na utulivu. Njiwa anashiria amani na anasimamia juhudi za kuitafuta amani katika shairi hili ukurasa wa kwanza ubeti wa kwanza unadhihirisha;

*Walinipa jina njiwa, ndege* ***mpole*** *nalia,*
*Njiwa nimetunukiwa,* ***wema*** *wa kuajabia,*
*Duniani natumiwa,* ***amani*** *kuashiriwa,*
*Njiwa ni utakatifu, ishara ya* ***utulivu****.*

Katika shairi soma katika diwani nachora kwa maneno mtunzi ametumia maneno soma, asubuhi na jioni ubeti wa tatu kumaanisha kila wakati mtoto asome asichague wakati bali awe na tabia ya kusoma kila wakati. Soma popote ulipo, hili tia mwako akilini ubeti wa nne akimaanisha azingatie na kutilia maanani masuala ya kusoma kila wakati. Tazama ukurasa wa kwanza ubeti wa kwanza.

*Soma, asubuhi na jioni,*

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Dkt. Jackline Murimi*
https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||


*Soma, kila kisomwacho, nje na ndani,*
***Soma, usichoke, ukajatia vyanda mdomoni.***

Katika shairi "Ajira kwa mtoto", mtunzi anarudia hoja moja kwa kutumia maneno tofauti ili kusisitiza pale anaposema ni wadogo kwa umri na miaka yao ni michache. Mtunzi amerejelea dhana moja kwani umri ni saw ana miaka. Mbinu hii imetumika kuleta msisitizo ambao ni muhimu kuwasilisha ujumbe kwamba watoto hao hawana uwezo wa kufanya kazi za sulubu kama wanazopewa. Tazama ukurasa wa tisa (u.b 1);

***Ni wadogo kwa umri***
*Miaka yao michache*

**Tamathali za Usemi**

Wamitila (2008) anasema kuwa ushairi ni Sanaa inayotumia lugha kwa ufanifu ikilinganishwa na tanzu nyinginezo. Mtunzi hutumia mbinu za matumizi ya lugha ambazo kimsingi zinahusu ukiushi na ukiukaji wa aina fulani ambapo neno au kifungu fulani hutumiwa kwa maana ya ziada ambayo ni tofauti na maana ya kimsingi. Hii ni kumaanisha kwamba tamathali hufafanua zaidi suala na kulithibitisha. Baadhi ya tamathali mtafiti alizochanganua ni maswali ya balagha, anafora, uhaishaji, takriri, tashbihi na nahau.

**Maswali ya Balagha**

Leech (1983) anaeleza kuwa maswali ya balagha ni maswali yanayotarajiwa kuwa na majibu mahsusi yenye muundo wa swali lakini yasiyotarajiwa kujibiwa.Maswali haya huwafanya wanaosoma kazi husika kutafakari,kushawishiwa na kuibua hisia.Maswali haya hupitisha ujumbe na kumhusisha msomaji.Mara nyingi majibu ya maswali ya balagha huwa ni dhahiri na mtunzi hutaka msomaji ajaze pengo hilo mwenyewe.Maswali haya humfanya msomaji kukubaliana na mtunzi kwani humshawishi.Kulingana na Wamitila 2008;19 maswali ya balagha hukikweza kiwango cha uhisivu katika kazi ya sanaa pamoja na kumhusisha msomaji katika hatima au jaala ya wahusika wanaopatikana katika kazi ya fasihi.Katika diwani mashairi ya Wanyama ya Ali Hassan Kauleni na Elvera Shabiha watunzi hawa wametumia maswali ya balagha. Kwa mfano tazama ukurasa wa tisa shairi "ndovu" (u.b1)

*Nitazame mwenye nguvu, masikio yaoneni,*
*Ninaishi nchi kavu, hula nyasi na majani,*
*Mkonga ninao ndovu, na pembe mbili usoni,*
***Ndovu na ukubwa wangu, nani asiyenijua?***

Katika kibwagizo hiki ndovu anauliza nani asiyenijua? Lengo lake ni kumshawishi msomaji kukubali kwamba yeye ndiye mnyama mkubwa ardhini. Umaarufu wake udhahiri. Swali la balagha huwa jibu la swali ni lilo hilo. Kimsingi huwa si swali bali kauli iliyochukua umbo la swali. Ni bayana kwamba ndovu ndiye mnyama mkubwa zaidi ardhini. Katika shairi Nyoka ndani ya diwani mashairi ya Wanyama pia watunzi wametumia swali la balagha. Tazama ukurasa wa kumi na sita. (U.b 2)

*Nakaa kwenye kichaka, mwituni hata majini,*
***Ninaishi kwa mashaka, nyoka mwaniuliani?***
*Ngozi yangu mwaisaka, yawafaa naamini,*
*Nyoka msinichukie, sina uadui nanyi.*

Nyoka anauliza swali linalozua mjadala na kupitisha ujumbe wa kutaka kuhurumiwa. Lengo la nyoka hapa ni kuwasilisha lalama zake kwambaanadhulumiwa na anaomba kuhurumiwa. Mtunzi anafaulu kupitisha hisia za mnyama huyu kwamba anadhulumiwa na watu kwa kuuliwa. Hivyo watoto wanapata funzo la kuto muuwa

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Dkt. Jackline Murimi*

https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||


nyoka. Kupitia maswali haya mawili watunzi wamefaulu kukatiza maelezo mengi, hivyo kudhihirisha ushairi kama Sanaa itumiayo lugha ya mkato kuwasilisha ujumbe.

**Anafora**

Anafora kulingana na Wamitila (2003) ni aina ya takriri inayohusisha kurudia kwa neno au kifungu cha maneno mwanzoni mwa kila mshororo katika shairi ili kuleta mahadhi katika shairi Pamoja na kuibua hisia nzito alizo nazo mtunzi. Anafora ya kileksia hutambua bahari ua kikwamba ambapo neno moja hurudiwarudiwa mwanzoni mwa kila mshororo. Tazama shairi "soma" kwenye diwani" Nachora kwa maneno" ukurasa wa kwanza; neno soma limerudiwarudiwa katika kila mshororo wa beti zote;

***Soma!***
***Soma**, mwana*

***Soma,** mwana soma!*
***Soma**, asubuhi na jioni*

***Soma** kila kisomwacho, nje na ndani,*
***Soma**, usichoke, ukajatia vyanda mdomoni.*

***Soma** popote ulipo, hili tia mwako akilini*
***Soma**, hata iwe bure au walipia, uogelee maishani,*
***Soma**, yalo muhimu utambue haki, uwe na thamani,*
***Soma**, hamna mwisho wa kusoma, bembeani hadi kaburini*

Lengo la kurudia neno soma ni kusisitiza ujumbe wa shairi na kuibua hisia akilini mwa msomaji. Kurudia neno soma pia kunaleta mahadhi na kuonyesha udharura wa kusoma kwa mtoto. Urudiaji pia huleta matumaini ya mtunzi kwamba ujumbe wake utafikia mlengwa.

**Uhaishaji**

Hii ni mbinu ya kuhaisha,kunafsisha au kufanya kitu au kiumbe kisicho hai kuwa na sifa za viumbe hai au kiumbe mwingine kuwa na sifa za binadamu.Katika diwani mashairi ya Wanyama watunzi wametumia mbinu ya kuzipa sifa za uhai Wanyama wote hususan sifa ya kuongea.Katika shairi ukurasa wa kwanza njiwa anazungumza katika beti zote mbili kwa mfano ;Mshororo wa kwanza wa ubeti wa kwanza anasema "walinipa jina njiwa ,ndege mpole nalia" .Njiwa anaeleza jinsi alivyo mpole.Njiwa anadai wema wa kuajabia na kwamba dunia anasema anatumiwa kuashiria amani.Tazama ukurasa wa kwanza ubeti wa shairi "Njiwa" kwanza anavyosema;

***Walinipa jina njiwa, ndege mpole nalia,***
***Njiwa nimetunukiwa, wema wa kuajabia,***
***Dunia natumiwa, amani kuashiria,***
***Njiwa ni utakatifu, ishara ya utulivu.***

Shairi punda katika ukurasa wa tatu linatupa kilio cha punda kulamikia dhuluma na haki zake kutopewa. ubeti wa kwanza mshororo wa pili anasema" ingawa pia mwapenda kunitusi hadharani". Shairi mbwa katika ukurasa wan ne wa diwani hii pia mnyama huyu anasema katika ubeti wa pili kwamba" chakula mwanirushia kunifanyia dharau". Uhaishaji huu pia unaopatikana katika mashairi ya Wanyama unajenga dhana ya fantasia.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Dkt. Jackline Murimi*

https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*



Fantasia kulingana na Wamitila (2003) ni sawa na njozinjozi.Ni dhana inayotumiwa kuelezea kazi ya fasihi ambayo ina sifa ambazo zinakiuka uhalisi.Fantasia hutumika zaidi katika kazi za kinathari ambazo huwa na mandhari ya ajabu, matukio magumu kukubalika katika hali ya kawaida na hata wahusika wasioweza kupatikana katika uhalisia.Kulingana na Bakize(2014)mtoto huamini kuwa kila kitu kinawezekana.Akimuona mnyama,ndege,mdudu huamini anaweza kuongea.Kwa watoto wadogo ambao ndio wanaanza kujifunza kusoma wakiona paka,mbwa, kuku n.k humwongelesha hii inatokana na imani waliyonayo kila kitu kinauwezo wa kibinadamu.Ndiposa mtunzi wa kazi za watoto hulazimika kuvihaisha na kuvipa matendo ya kibinadamu vitu visivyo binadamu.Uhaishaji kama mbinu imefaulu kuwasilisha maudhui na kuwafanya walengwa wa mashairi haya kuuona ukweli na kuhusiana na wahusika ambao ni Wanyama.

**Takriri**

Takriri ni urudiaji wa sauti, neno au sentensi fulani. Urudiaji huibua hisia kwa wasomaji Urudiaji unaweza kujitokeza katika kiwango cha neno, sauti, vifungu, mshororo au maumbo. Huongezea nguvu au hata kuchukua mahali pa mizani. Urudiaji sauti mwishoni huunda urari wa vina. Huyafanya mashairi ya watoto kuimbika. Neno linaporudiwa rudiwa huonyesha kusisitiza kwa ujumbe fulani. Takriri hujenga wizani ya shairi husika. Kwa mfano katika shairi Samaki chakula bora katika ubeti wa pili.

*Samaki **kuogelea**, raha mwake **maishani**,*
*Mayai **yanaelea**, watoto toka **tumboni,***
*Huangua **kuenea**, wengineo **duniani***
*Hawana haja **kulea**, chakula chao **majini**,*
*Hula pia na **mimea**, kila siku wa **mbioni***
*Kula uujenge mwili, Samaki chakula bora.*

Vina vya kati ninarudia sauti -ea na vina vya nje vina sauti -ni. Ni dhahiri mtunzi ametumia sauti hizo ili kusisitiza ujumbe wa shairi hili, kuwezesha watoto kuimba na kujenga taswira kamili ya Samaki kuwa chakula bora kwa watoto.

**Tashbihi**

Kwa mujibu wa Leech (1969;74)tashbihi huwa na maana ya juujuu ikilinganishwa na jazanda ambayo huwa na maana ya ndani.Aidha ,tashbihi imedondoshwa kutoka kwa jazanda.Pia Kuhenga (1977;3)anasema tashbihi ni mtindo wa kiuneni wa kifani ambao kwao kitu kimoja au zaidi hulinganishwa au kufananishwa na kitu kingine tofauti.Mfanano huu ni wa kiutendaji au kimaumbile kama vile sura,rangi na jinsi ya kujimudu.Neno tashbihi limezaliwa kutoka kwenye neno shabihi ambalo lina maana ya kufanana au kulingana na.Msokile(1993;40)anasema tashbihi ni tamathali ya usemi ambayo huhusisha vitu ambavyo ni kizungumziwa,kifananishi na kiungo.Hivyo tashbihi lazima iwe na viungo vitatu.Wamitila ( 2003;222) anasema tashbihi ni tamathali ya usemi ambapo vitu viwili hulingaanishwa kwa njia waziwazi.Aidha hutambulishwa na viungo;kama,mfano wa,mithili ya, ja,kama vile sawa na .kadhalika

Hii ni mbinu ya kulinganisha vitu, watu, mahali, hali moja, moja kwa moja kwa kutumia maneno ya kulinganisha "kama", mithili" ya," sawa na "ja". Mtunzi ametumia tashbihi katika shairi 'Simu ya Mkononi' kwenye diwani "Nachora kwa maneno" tazama ubeti wa saba ukurasa wa kumi.

***Sauti zake ni nzuri, zalia kama muziki,***

*Zavutia kwa urari, milio mfano wa nyuki,*
*Zimekuwa mashuhuri, zachoma kama mkuki.*

Mtunzi anazilinganisha sauti za simu kuwa zalia kama muziki na pia anaufananisha umashuhuri kuwa unachoma kama mkuki.

**Nahau**

Msokile (1993) ana maoni ya kuwa nahau ni semi ambazo hutumiwa na mwandishi ili kutia nguvu na msisitizo katika maana,mtindo na pengine sauti katika maandishi.Nahau zinatumiwa pia kuipamba kazi ya sanaa ya kifasihi kwa kuongeza utamu wa lugha.Ngure(2011) amesema nahau ni misemo iliyojengwa kwa kutumia maneno ya kawaida lakini ambayo huwa imesetiri maana tofauti na ile iliyobebwa na maneno yayo hayo katika matumizi yake ya kawaida.Guantai(2002) amesema ya kwamba nahau ni mafungu ya maneno yaliyopewa maana maalum na jamii.Nahau hutumika kwa njia ya kupamba kazi ya fasihi kama mashairi ya watoto.Nahau pia hutumiwa na wasanii na wazungumzaji kuyakazisha maelezo yao.Kulingana na Wamitila (2010) Nahau hutumiwa kuelezea mbinu za matumizi ya lugha ambazo kimsingi zinahusisha ukiushi wa aina fulani ambapo neno au kifungu fulani hutumiwa kwa maana ambayo ni tofauti na maana ambayo ni tofauti na maana ya kimsingi.Nahau katika fasihi ya watoto hutumika kukuza lugha.Vilevile nahau hutumiwa kupamba lugha.

Ni fungu la maneno linalotumika kutoa maana nyingine badala ya ile maana ya maneno yaliyotumika. Nahau huwa na vitenzi. Katika shairi" Soma" katika diwani "Nachora kwa maneno" la Swaleh mdoe tazama ukurasa wa kwanza ubeti wa tatu mtunzi anasema 'soma usichoke, ukajatia vyanda mdomoni'.

*Soma, asubuhi na jioni,*
*Soma, kila kisomwacho, nje na ndani,*
*Soma***, ***usichoke* ***ukajatia vyanda mdomoni.***

Nahau hii ina maanisha kujuta na kujilaumu kwa masaibu yatayokupata kwa kutozingatia elimu. Nahau ukajatia vyanda mdomoni ina maanisha mtunzi ana muonya mtoto asome na kuzingatia msomo asije juta siku za usoni. Katika ubeti wa nne mtunzi anamshauri mtoto kusoma popote alipo na kushika sana asomacho. Katika ubeti wanne wa shairi hilo pia mtunzi pia ametumia nahau "tia akilini" "uogelee maishani "na "bembeani hadi kaburini' kama inavyodhihirika ukurasa huo wa kwanza ubeti wa nne;

*Soma, popote ulipo,* ***hilitiamwakoakilini****,*

*Soma, hata iwe bure au walipia,* ***uogeleemaishani,***

*Soma, yalo muhimu utambue haki, uwe una thamani,*

*Soma***, ***hamnamwishowakusoma***, bembeani hadi kaburini.***

Kutia "mwako akilini" ina maana kumbuka kila wakati kuwa masomo ni muhimu kwako."Uogelee maishani "ina maana elimu itakupanulia mustakabali wako na "bembeani hadi kaburini" ina maanisha maisha yako yote zingatia elimu.

**Toni ya Mashairi Teule**

Wamitila (2003) anaeleza toni kuwa usikikaji wa sauti ya ushairi. Usikikaji huo unaweza kuathiri ujumbe kwa kusisitiza au hata Kwenda kinyume chao. Toni inahusu kuchunguza namna mtunzi anasema jambo fulani, jinsi shairi hilo litakavyosikika ikiwa litasomwa hadharani.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Dkt. Jackline Murimi*

https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||


Arege (2013) anasema Toni ni hisia za nafsineni zinazoibuka kutokana na uteuzi wa mtunzi wa maneno. Zipo toni za kubeza, kuchekesha, kuhoji na kulalamika. Toni ya shairi inafungamana kwa kiasi kikubwa na masuala anayozungumzia mshairi. Katika shairi" Ukame" katika diwani" 'Nachora kwa maneno" mtunzi ameandika kwa toni ya kusikitisha na kuomba msaada Tazama ukurasa wa saba. (u.b 5)

*Chochote hata muhogo, toa usione soni,*

*Haba na haba kwa gogo, njaa tutaipigeni*

*Chako na changu kidogo, uhai tuokoeni,*

*Ukame umeingia**, shimetusaidiane**.*

**Vielelezo vya Picha na Michoro ya Mashairi Teule**

Bakize (2014) Vielelezo vya picha au michoro humfanya mtoto avutiwe zaidi na kuwa makini na ile kazi ya fasihi na kuona uhalisia wa kile anachokisoma, pia humfanya mwandishi kujiaminisha na kile anachokiwakilisha kwa hadhira yake ya watoto. Picha huwasilisha ujumbe kwa uasilia na kwa njia ya moja kwa moja. Picha husaidia kuuelewa ulimwengu wanamoishi kwa wepesi kwa sababu hupenda kuona, kusikia milio, kuona vitu, kunusa harufu, kugusa na si kwa maneno matupu.

Crystal na Davy (1969)wanasema kwamba matumizi ya sauti na michoro yenye maumbo maalum hudhihirisha ujumi,uhalisia na ufafanuzi zaidi kuhusu ujumbe unaopitishwa na mwandishi katika kazi ya fasihi.Aidha Pierce (1977:28) alithibitisha matumizi ya ishara alipoangazia nadharia ya ishara katika kazi za fasihi.Alisema kwamba ishara huonyesha uhusiano uliopo kati ya kiashiria na kiashiriwa.Alibainisha vitengo vikuu vya ishara,mathalan,ishara halisi ambazo zinaweza kuwa ni sifa ,kanuni,desturi au tabia za kitu chenyewe.Pia ishara ambazo zina husishwa na viashiriwa.Aidha ni uhusiano uliopo kati ya kiashiria na kiashiriwa.Katika kitengo cha pili,alibainisha ishara katika vikundi vitatu;picha au michoro ,kielelezo cha sifa au tabia na mfumo wa alama zinazowakilisha kundi fulani la mawazo.Goins (2004) anaongezea kuwa picha huchochea uwazaji razini na wa kihakiki wa mtoto kwa kumpa habari muhimu ambazo anaweza kuzitumia kulinganisha alichokisoma na anachokiona au kile amewahi kukipitia. Katika uchanguzi huu mtafiti amebainisha kwamba mashairi yote teule yamewekwa na michoro katika diwani zote mbili zinazochanganuliwa.

Katika diwani "*Nachora kwa maneno"* ya Swaleh Mdoe katika ukurasa 1, mtunzi amechora picha ya kijana aliyetia vidole mdomoni. Ni wazi kwamba mtunzi anarejelea onyo lake kwa mwana kuzingatia masomo au aje kujitia vyanda mdomoni akimaanisha kujuta. Mtunzi anasisitiza kwamba kutozingatia masomo huleta majuto. Chambilecho wahenga majuto ni mjukuu huja baadae.

Katika shairi "Ukame" kwenye diwani '*Nachorakwamaneno'* pia kuna michoro ya kusikitisha. Shairi liko ukurasa wa saba . Kuna mchoro wa mti uliokauka, ngombe aliyekonda akionekana kuchunga mahali pasipo na nyasi zozote. Tatu kuna mchoro wa ngombe aliyeaga na mifupa imebaki ardhini ilhali kuna mwingine amelala ardhini akionekana kushindwa kutembea kwa makali ya ukame .Kuna mchoro wa binadamu aliyedhoofika sana kiasi cha kushindwa kutembea kabisa anaonekana akitambaa,ndege wa kula mizoga anaonekana akimnyemelea ishara kwamba anataka kumla atakapoaga.Athari za ukame zinadhihirishwa na michoro hii.Michoro hii inaleta hisia za kusikitisha ,kuatua moyo pakubwa.Picha hizi zinafaulu kuwasilisha ujumbe wa mtunzi kwamba nchi imepata janga na shime watu wasidiane kuyazuia maafa.

Kaika shairi "Ajira kwa watoto' ukurasa wa tisa katika diwani "Nachora kwa maneno" ya mtunzi Swaleh Mdoe amechora picha za watoto wawili wakifanya kazi. . Ni bayana kwamba mtunzi amezichora picha hizi

kuusukuma ujumbe wake kwamba watoto wanafanyishwa kazi za sulubu. Mchoro mmoja mtoto anaonekana akivunja mawe kutengeza kokoto ilhali picha ya pili akichimba kwa jembe ishara ya kazi ya shambani ya kulima. Mtunzi ametumia michoro kuusisitiza ujumbe wa kutowaajiri watoto.

Katika Shairi "Simu ya mkononi" katika ukurasa wa kumi katika diwani "Nachora kwa maneno" ya Swaleh Mdoe mtunzi amechora michoro akirejelea yaliyomo kwenye shairi hili. Michoro ya kwanza ni ya mtu wa jinsia ya kiume na wa jinsia ya kike wakipiga simu za mkononi. Mchoro wa pili ni wa mtambo wa setilaiti inayotumika katika mawasiliano ya simu vile vile mtunzi anamchoro wa dereva anayeonekana kuitazama simu yake ya mkononi. Huyu dereva anatajwa katika ubeti wa tano kwamba aache kuzungumza kwa kutumia simu anapoingia garini. Anashauriwa simu aikomeze hadi atakaposimama.

Michoro hii muhtasari faafu wa ujumbe wa mtunzi kwa watoto.Michoro ya Samaki mbalimbali katika ukurasa wa 12 na 13 wa diwani *Nachora kwa Maneno* pia inafaulu kupanua muktadha na uelewa wa mtoto ambaye ndiye mlengwa katika shairi Samaki chakula bora. Mtunzi amefaulu kuchora aina tofauti za samaki aliowataja kwenye shairi lake. Goins (2004) anasema Picha zilizomo huwa kama makavazi ya kiakili ya mtoto. Wakati ambapo mtoto atakuwa amesahaua aina za Samaki basi michoro itamsaidia kukumbuka majina yao. Michoro hii ni ya kiboma, pono, papa na jodari.

Diwani "*Mashairi ya wanyama*" ya Ali Hassan Kauleni na Elvera Shabiha imetumia michoro ya wanyama kwa kila shairi ili kuwapa watoto nafasi ya kutalii kwa undani maana na ujumbe unaowasilishwa na mtunzi. Shairi "Njiwa" ukurasa wa kwanza linaukokoteza ujumbe wa njiwa kuwa mpole na anaye ashiria amani. Njiwa ni ndege anayetumika kuwasilisha ujumbe wa amani hasa kwa watoto na taifa lote kwa jumla.

Shairi "punda" katika ukurasa wa tatu diwani "Mashairi ya wanyama" pia lina mchoro wa punda. Watunzi wamechora punda akiwa amebebeshwa mizigo kuashiria dhuluma na unyanyasaji wa Wanyama.Michoro huwapa watoto nafasi ya kutalii kwa undani masuala mbalimbali n ahata kuibua maana kadhaa wanapoichunguza. Kwa njia hii, wanaweza kufikiria kwa ubunifu na umakini hata kuibua mijadala zaidi kuhusu shairi husika. Picha ya punda kubebeshwa mizigo inazua mjadala kuhusu haki za Wanyama pia.

Shairi "Mbwa" katika ukurasa wa nne diwani "Mashairi ya wanyama" watunzi wameweka mchoro wa mbwa sifa za mnyama huyu zimeelezwa kwenye shairi hili vizuri, mwandani, mwenye vipaji adimu na mwaminifu kwa binadamu. Sifa za mhusika mbwa zinapigiwa upondo na mchoro. Mtoto anapoitazama na kuimithilisha na mnyama halisi basi sifa zinazorejelewa huingia kwenye akili na kumfaa mtoto anayesoma shairi na kuiona picha rejelewa.

Hoopes (1991) anasema kwamba ishara za picha kilelezo cha sifa ni mfano wa alama zinazowakilisha kundi fulani la mawazo huonyesha namna ishara zinazoonekana zinavyosheheni ujumbe wa kidhahania.Aidha ishara hizi humsaidia mtafiti kutafakari zaidi kuhusu ujumbe unaowakilishwa na ishara hizo.Katika shairi ndovu ukurasa wa tisa (tazama hapo chini) watunzi wanatoa lalama za ndovu kwamba anawindwa kwa pembe zake.Wanaozipata pembe hizo hupata madola lakini hufungwa jela.Ndovu anazua mjadala wa uwindaji haramu na faida zake.Wawindaji hufaidika kwa kupata madola na kuchangia kuuwa utalii.Ndovu katika shairi hili anadai hali paa wala swara lakini mchoro unabainisha kwamba ni mharibifu mazingira kwani amechorwa ameuangusha mti. Wanasayansi wanasema ndovu huangusha miti ili apate chakula chake ambacho ni majani, matawi na maganda ya miti. Wananguvu za kuangusha miti mikubwa ili wapate chakula hicho. Picha hii ya ndovu imefaulu kuleta mjadala mwingine kando na ule wa uwindaji haramu. Mchoro huu umefaulu kuteka nadhari ya msomaji ambaye katka muktadha huu ni mtoto na kumpa nafasi ya kutafakari zaidi ujumbe unaowasilishwa na mshairi. Picha hii inazua mjadala wa uhifadhi wa misitu katika mazigira anamoishi ndovu kwani ni dhahiri kwamba huharibu mazingira kwa kungoa miti.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Dkt. Jackline Murimi*

https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||


Katika shairi "Nyoka" lililo katika diwani "Mashairi ya Wanyama" tunapata mchoro wa nyoka akiwa amejizungusha kwenye tawi la mti. Ukurasa wa 16 Watunzi wanaeleza lalama za nyoka kutaka kuhurumiwa akidai anadhulumiwa kwa kupondwa. Freeman (2007) anasema kwamba athari ya ishara za picha katika ushairi ni kuzua falsafa, hisia na picha au taswira katika lugha ambazo huwezesha akili ya mshairi au msomi kukubaliana nazo kama matukio halisi. Shairi nyoka linazua hisia na mjadala, nyoka analamikia kuuliwa na binadamu lakini ni wazi kwamba pia yeye humuua binadamu kutokana na sumu kali anapomuuma binadamu. Jackson (2014) anasema kwamba nyoka aitwaye Inland taipan ndiye mwenye sumu zaidi kwani anasumu kali na anapouma huachiliza sumu nyingi zaidi. Mchoro wa nyoka uliochorwa na ujumbe wake katika shairi vinazua mjadala wa umuhimu wa nyoka katika maisha ya binadamu ambalo ni funzo muhimu kwa watoto wa shule kuhusu uhifadhi wa Wanyama kama nyoka.

**Urudiaji**

Watunzi wa diwani zote mbili wametumia mbinu ya urudiaji katika mashairi teule. Urudiaji unadhihirika katika vina vya kati vya mashairi yote na vina vya nje vya mashairi yote. Vile vile urudiaji wa kibwagizo unadhihirika katika mashairi mengi. Kwa mfano shairi Ukame ukurasa wa 7 katika diwani nachora kwa maneno ubeti wa pili vina vya kati ni ma -na vya nje ni- ka. Kibwagizo nacho ni ukame umeingia, shime tusaidiane. Katika ubeti wa 5 wa shairi hilo vina vya kati ni -go na vya nje – ni. Katika diwani Mashairi ya Wanyama Punda ubeti wa kwanza vina vya kati ni -nda na vya nje ni – ni Ubeti wa pili vina vya kati ni- sha, na vya nje -ngu. Kibwagizo cha shairi hili ni Punda nina zangu haki, komeni kunidhulumu. Urudiaji wa vina vya mashairi teule na vibwagizo umechangia katika kufanya mashairi haya kuweza kuimbwa kwani urudiaji umeleta mahadhi. Urudiaji wa kibwagizo umeleta msisitizo wa ujumbe wa mashairi teule. Kwa mfano shairi" Nyoka" katika diwani mashairi ya wanyama ukurasa wa 16 kibwagizo **'Nyokamsinichukie, sina uadui nanyi."**

*Nyoka sitaawaacha nyuma, katika ukumbi huu,*

*Kwa hasira nasimama, ingawa sina miguu,*

*Mwanifanyia dhuluma, mwaniponda kwa miguu,*

***Nyoka msinichukie, sina uadui nanyi.***

*Nakaa kwenye vichaka, mwituni hata majini,*

*Ninaishi kwa mashaka, nyoka mwaniuliani?*

*Ngozi yangu mwaisaka, yawafaa naamini,*

***Nyoka msinichukie, sina uadui nanyi.***

**Taswira**

Kulingana na Wamitila (2003) taswira ni dhana inayotumiwa kueleza neno,kirai au maelezo ambayo yanaunda picha fulani katika akili ya msomaji.Taswira zinaweza kuwa za kimaelezo yaani maelezo fulani yakaunda picha au za ki-ishara zinazounda picha ambayo inaashiria jambo fulani au imeficha jambo fulani.Kulingana na Kahigi na Mulokozi taswira ni mbinu ya matumizi ya picha katika utungo na katika mawazo ya msimaji utungo huo .Aidha ,picha ni matumizi ya lugha yanayopambanuliwa na uteuzi mzuri wa maneno ,uangalifu na udhahiri wa maelezo yenye kuhusisha na kujumuisha dhana moja ili kuleta taswira na athari maalum katika mawazo ya msomaji.King'ei na Kemoli (2001;58) wanasema kuwa mshairi mara nyingi huunda taswira ili kumpa msomaji picha kamili kimawazo za yale anayosimulia. Isitoshe, picha hizi huweza kufafanua tukio, hali fulani

ya mhusika au kisa fulani. Mshairi mbunifu hutumia taswira ambayo inaonekana waziwazi na huitumia kwa ukamilifu katika kujenga utajiri na uzito wa maudhui ya shairi lake. Matumizi mazuri ya taswira humfanya msomaji aulewe ujumbe wa shairi.Katika diwani nachora kwa maneno mtunzi Swaleh mdoe ametumia taswira kurahisisha uelewekaji wa janga la ukame(uk7) lililoikumba Kenya.Mtunzi amelenga kuwarai wakenya kusaidia wengine kwani madhila ya ukame ni makubwa mno.Maelezo na michoro ya shairi hili yanatupa hisia fulani kutokana na uhalisia wa hali halisi ya ukame ulioikumba nchi.Kulingana na Senkoro(1988;41)taswira zaweza kugawanywa makundi matatu;taswira zionekana,taswira za mawazo na taswira za hisi.Taswira hizi zinaweza kutambulika katika shairi moja au mashairi tofauti. Mwongozo huu wa Senkoro tutautumia katika kuchanganua taswira zinazojitokeza katika mashairi ya diwani hizi mbili.

**a. Taswira zinaonekana.**

Watunzi wametumia michoro kujenga taswira mbalimbali. Mchoro wa punda katika diwani mashairi ya wanyama ukurasa wa tatu ni mfano faafu. Taswira hizi zinadhihirika katika mashairi kama soma katika diwani nachora kwa maneno uk 1.Mchoro wa mtoto aliyejitia vidole mdomoni.Vilevile michoro katika ukurasa wa 7 wa diwani "Nachora kwa maneno" wa shairi ukame unadhihirisha mashaka ya janga la ukame nchini.Mti uliokauka ,ng'ombe iliyokonda kiasi cha mbavu zake kuonekana,mtoto aliyekonda mbavu zaonekana ni thibitisho la taswira ya kutamausha inayoonekana.Shairi ajira kwa watoto ukurasa wa 9 diwani nachora kwa maneno pia lina taswira ya kuonekana pale michoro ya watoto wanaovunja mawe wanachorwa wakivunja mawe.Shairi Simu ya mkononi ukurasa wa 10 ndani ya Diwani nachora kwa maneno lina mchoro wa dereva akiwa ameikodolea macho simu yake ya mkononi.Shairi Samaki chakula bora ukurasa wa 12 na 13 pia katika diwani hiyo lina michoro ya aina tofauti za samaki. Samaki kama chakula bora wameainishwa kwa sifa zao tofauti. Picha zinathibitisha maelezo ndani ya shairi kwa mfano Pono anasifika kuwa na minofu ub 4 mshororo wa tano.'pono naye akiwepo, minofuye nilaini. Mshairi kupitia kwa mchoro na maelezo tunapata picha ya Samaki pono alivyo na minofu. diwani mashairi ya Wanyama watunzi wameweka vielelezo vya michoro ya Wanyama katika kila shairi husika kujenga taswira ya muonekano ili kuwasilisha maudhui mbalimbali.Kwa mfano ukurasa wa kwanza ndege .Katika njiwa amechorwa kusisitiza ujumbe wa amani kwa kujenga taswira kutokana na muonekano wake.Shairi punda ukurasa wa tatu una mchoro wa punda kabeba mizigo unajenga taswira ya muonekano w kuteswa na kudhulumiwa kwake.Shairi mbwa lina mchoro wa mbwa kuleta taswira ya mwandani wa binadamu na uaminifu kwake.Ndovu pia amechorwa katika shairi ndovu ukurasa wa tisa kuleta taswira ya mnyama mkubwa zaidi ardhini.Mwisho shairi nyoka ukurasa wa 16 pia lina mchoro wa nyoka kuchangia maudhui ya huruma.Michoro iliyotumika imefaulu kuwasilisha maudhui yaliyozungumziwa na watunzi kikamilifu.Picha hizi zote ni faafu katka kujenga taswira zinazoonekana.Shairi" Punda" katika Diwani mashairi ya Wanyama u.k 3 lina picha ya punda aliyebebeshwa mizigo mikubwa iliyojaa mgongo wote.

**b. Taswira za mawazo**

Taswira hizi huwazika tu na humfanya msomaji kutafakari kinachozungumziwa na mshairi. Kulingana na Kuvuna, Mvati na maliachi (1992;26) taswira za kimawazo huelezwa kwa kutumia hali dhanifu za kufikiria tu.Katika shairi "Simu ya mkononi" ndani ya Diwani 'Nachora kwa maneno" mtunzi anatutahadharisha kuhusu utumiaji wa simu ndani ya ndege kwa kudai itatoa cheche. Maelezo haya ni ya kidhanifu tu. Tazama ukurasa wa kumi (Ub 3)

*Kwenye ndege uizime, simu yako isiseme,*

***Hatari kama umeme, yaweza kutoa cheche,***

*Wanawake kwa wanaume, onyo hili msikize.*

**IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH**
**(ISSN: 2805-413X)** **Dkt. Jackline Murimi***

https://ijojournals.com/ *Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||*



Mshairi anamwacha msomaji katika hali ya kutafakari kuhusu hatari ya kutumia simu akiwa ndani ya ndege. Msomaji anajengwa na mawazo ya kuhofia hatari kubwa ya kutumia simu kwamba inaweza kuzua baa la moto ambao utaleta maafa. Taswira za mawazo pia zinabainika katika shairi "Punda" kwenye diwani" Mashairi ya Wanyama" ukurasa wa tatu ubeti wa pili punda anasema;

***Mizigo mwanibebesha, hiyo ndiyo kazi yangu,***

***Nabeba bila kubisha, maji mgongoni mwangu,***

*Lakini mkinichosha, hurusha mateke yangu,*

*Punda nina zangu, komeni kunidhulumu.*

Punda analalamikia kubebeshwa mizigo, maji mgongoni anabeba bila kubisha. Anapoona mateso haya yamezidi basi hurusha mateke. Mnyama huyu analalamikia kwa uzito wa kazi anazopewa. Anaomba asidhulumiwe na kuteswa. Taswira ya mawazo inadhihiria kwa msomaji wa shairi hili kutokana na maneno ya punda.

**c. Taswira za hisi**

Senkoro ( 1988)anaeleza kuwa taswira za hisi zina nguvu kubwa ya kuganda akilini na kunasisha ujumbe kwa wasikilizaji au wasomaji wa shairi.Taswira ya hisi huibua hisia kwa msomaji hasa za ndani.Hisia hizi aghalabu zaweza kuwa wasiwasi,woga hasira,kinyaa,huruma ,kusikitika na kadhalika.Hisia hizi humfanya mhusika kuwa na msukumo wa kutenda kitu fulani.Anaweza kuamua kuteta,kupiganaau kujiepusha.Vitendo hivyo ni matokeo ya msisimko alioupata iwe huzuni,hasira,chuki na kadhalika.Katika mashairi teule watunzi walitumia taswira hisi kudhihirisha hisia mbalimbali.Katika diwani "Nachora kwa maneno" shairi 'Ukame' ukurasa wa 7 ubeti wa nne mtunzi anaeleza jinsi watu walivyoathirika na ukame anaposema kwa hisia hizi ;

*Tumeyaona kwa kicho, **maafa** haya jamani,*
***Watu wanakufa nacho, ni mbavu tupu mwilini,***
***Wameyakodoa macho, wafa wakijionea,***
*Ukame umeingia, shime tusaidiane.*

Katika ubeti huu mtunzi analeta hisia za kusikitisha kwani maafa na watu kuwa mbavu tupu mwilini inasikitisha. Kukodoa macho huku wanakufa inatia huzuni kwa msomaji. Katika diwani mashairi ya Wanyama shairi" Nyoka" lina kilio cha nyoka akilalamikia anavyofanywa na watu. Tazama nyoka anavyolalamika katika ukurasa wa 16 ubeti kwanza anadhihirisha wazi hisia kwa kusema;

*Nyoka sitawachwa nyuma, katika ukumbi huu,*

***Kwa hasira nasimama. ingawa sina miguu,***

***Mwanifanyia dhuluma, mwaniponda kwa miguu,***

*Nyoka msinichukulie, sina uadui nanyi.*

Nyoka anazua hisia za huruma anaposema mwanifanyia dhuluma mwaniponda kwa miguu na nyoka msinichukie sina uadui nanyi. Hisia za kumhurumia nyoka zinajengwa na lalama zake kwamba asichukiwe kwani si adui. Mtunzi amefaulu kuzua hisia.

## Hitimisho

Utafiti umebaini kwamba mashairi ya watoto yanafaa katika kufundisha maadili mema na kuwasaidia watoto kukua katika jamii inayowajali. Hata hivyo, watunzi hawajazingatia masuala ibuka katika elimu ya maadili kama vile ushoga, usagaji, na ndoa za jinsia moja. Badala yake, wamezingatia maadili kama huruma, upole, uaminifu, na kujali wanyama. Pia, watoto wanapaswa kufunzwa kuhusu uhifadhi wa wanyama, mfano nyoka, na umuhimu wa mazingira ili kuondoa hisia hasi kuhusu wanyama. Mikakati kama upandaji miti ni hatua nzuri katika kukabiliana na athari za ukame. Teknolojia ya kisasa inahitaji ufahamu wa matumizi salama, kama kutopiga simu wakati wa kuendesha gari.Lugha inayotumika katika mashairi inawafaa watoto, na watunzi wametumia mbinu mbalimbali kama nahau, taswira, na toni kuwasilisha jumbe zao, hivyo kuchochea uelewa wa maudhui.

## Mapendekezo

Jamii inakabiliwa na matatizo mapya ya kimaadili, na ni muhimu kwa watunzi wa mashairi ya watoto kuandika kuhusu masuala haya, ikiwa ni pamoja na kupinga itikadi kali za kidini na ndoa za jinsia moja. Utafiti huu unashughulikia maudhui, wahusika, na mitindo katika fasihi ya watoto, na inapendekezwa utafiti zaidi ufanywe kuhusu mitindo ya mashairi, athari za vielelezo vya picha, na maudhui mtambuka ya kisasa. Pia, ni muhimu kufanywa tafiti kuhusu usawiri wa wahusika katika diwani nyingine za watoto.

## Marejeleo


Coombes, H. (1991). *Literature and Criticism*. 160. Retrieved from https://books.google.com/books/about/Literature_and_Criticism.html?id=vJovAQAAIAAJ

Gituru, M. W. (2019). *Unyambulishaji wa Vitenzi Katika Kigĩchũgũ* (Doctoral dissertation, Chuka University).

Ismail, F. H. (2019). *Kuchunguza Mtindo na Dhamira katika Tamthiliya ya Mondlane na Samora* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).

Kimetto, H. K. (2016). *Ulinganifu Wa Taarifa Za Habari: Tathmini Ya Tafsiri Kutoka Kiswahili Hadi Kikipsigis Katika Kituo Cha Kitwek* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).

Massoud, S. S. (2018). *Kutathmini Matumizi ya Mtindo na Dhamira katika Tamthiliya za Mashetani na Mashetani Wamerudi: Utafiti Linganishi* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).

Mwangi, P. K., & Munyao, J. K. (2016). Mtindo na Maudhui katika Nyimbo za Kisiasa za Msanii John De'Mathew nchini Kenya. *Mulika Journal*.

Nguti, M. (2013). *Ulinganishi Wa Matumizi Ya Tasfida Za Muktadha Wa Nyumbani Katika Lugha Ya Kikamba Na Kiswahili* (Doctoral dissertation).

Nyandiwa, H. (2015). *Uchanganuzi Wa Kimtindo Wa Zinguo La Mzuka Na Mbaya Wetu* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).

Nyutu, J. (2016). *Mtindo Katika Kazi Za Kubuni Za Leonard Sanja* (Doctoral dissertation, University of Nairobi).

Stephano, R. (2022). Ukubalifu wa Tafsiri za Kitamaduni: Mfano wa Tafsiri ya Filamu ya Yesu kutoka Kiingereza kwenda Kinyaturu. *Mulika Journal*.

IJO - INTERNATIONAL JOURNAL OF EDUCATIONAL RESEARCH
(ISSN: 2805-413X) Dkt. Jackline Murimi*
https://ijojournals.com/ Volume 07 || Issue 10|| October, 2024 ||


Tutaş, N. (2006). Critical thinking through literature. *Ankara Üniversitesi Dil ve Tarih-Coğrafya Fakültesi Dergisi*, *46*(1), 93-108.

Wamitila, K. W. (2003). *Kichocheo cha Fasihi: Simulizi na Andishi*. 264. Retrieved from https://books.google.com/books/about/Kichocheo_cha_fasihi.html?id=6qcaAQAAIAAJ

Wamitila, K. W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Retrieved from http://erepository.uonbi.ac.ke/handle/11295/46826

Yunus, M. K. (2013). *Masuala ya Kisiasa Katika Ushairi wa Kandoro: Mifano Kutoka Katika Mashairi Yake* (Doctoral dissertation, The Open University of Tanzania).